**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**640** **HISABATI**

**Muda: Saa 3 Hours** **Mwaka: 2024**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**


Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Toa sababu nne za wafanyabiashara kutoka bara la Ulaya kuwa miongoni mwa vitangulizi vya ukoloni.
2. Eleza athari za utawala wa moja kwa moja kwa jamii za Kiafrika.
3. Pambanua kwa kifupi majukumu ya mashirika manne ya Umoja wa Mataifa kwa wanachama wake.
4. Eleza umuhimu wa Azimio la Kazi, Andalio la somo, Shajara ya somo, na Nukuu za somo kwa mwalimu anayefundisha somo la Historia.
5. Eleza kwa ufupi tofauti kati ya nadharia ya uumbaji na nadharia ya mabadiliko ya kimaumbile.
6. Eleza kwa kifupi vigezo vinne ambavyo mwalimu anaweza kuvitumia katika uchaguzi wa zana ili aweze kufikia malengo ya somo wakati wa kufundisha.
7. Eleza kila moja ya magimba ambayo ni;
   (a) Satelaiti
   (b) Asteroidi
   (c) Kometi
   (d) Vimondo
8. Eleza kwa ufupi athari nne zinazojitokeza hapa duniani kudhihirisha uwepo wa mizunguko miwili ya sayari dunia.
9. Fafanua kwa ufupi sababu nne zinazopelekea kuwepo kwa tofauti za tabianchi nchini Tanzania.
10. Eleza kwa ufupi sifa nne za mistari ya kontua kama inavyotumika katika uchoraji wa ramani.

**SEHEMU B (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Shamba la Chuo cha Ualimu Amkeni lina umbo kama inavyoonekana kwenye mchoro ufuatao: Je, shamba hilo lina eneo la kiasi gani?





Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

12. Walimu tarajali walikuwa wakifanya mazoezi ya kutafuta kikamilisho cha seti, muungano na muunganiko wa seti mbalimbali:

(a) Iwapo $\mu = \{1,2,3,4,5,6,7,8,9\}$ na $A = \{5,7,8,9\}$ walipata nini katika seti zifuatazo?

(i) $A'$

(ii) $A' \cup A$

(iii) $A' \cap A$

(b) Utatumiaje set $\mu=\{1,2,3,4,5,6\}$, $A=\{1,2,3,4\}$ na $B=\{2,3,4,5,6\}$ ili kuonesha kwamba:

(i) $(A \cap B)' = A' \cup B'$ ?

(ii) $(A \cup B)' = A' \cap B'$ ?

(iii) $(A')' = A$

13. Matokeo ya upimaji wa kielimu ni muhimu kwa sababu huonesha mafanikio na mapungufu kwa wadau mbalimbali wa elimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kwa kutumia wadau watano, eleza namna wanavyonufaika na upimaji huo.

14. Walimu wa Hisabati wanatakiwa kuwaandaa wanafunzi kusoma kwa vitendo, nadharia na kutumia Hisabati katika maisha ya kila siku ili wasiaminishwe kuwa somo hili ni gumu na halina manufaa. Tetea kauli hii kwa kutoa hoja tano.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org